# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA AFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Mheshimiwa Spika,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa utukufu na rehma, kwa kutujaalia uzima na Afya njema, na kuweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa, kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha nakushukuru na kukupongeza wewe **Mheshimiwa Spika,** kwa namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi mkubwa kwa kipindi chote cha mwaka mzima, ni imani yangu kwamba, utaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha wananchi.

Mheshimiwa Spika,

Nachukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuiongoza nchi yetu, kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa aliounesha kwa kipindi chake cha kwanza cha uraisi, na hiki anachoendelea nacho. Hekima na Busara zake anazozitumia katika

kuongoza nchi yetu, ndizo ambazo zimetufanya hadi leo kuweza kuishi katika nchi yetu kwa amani na utulivu.

Sina budi pia kumshukuru na kumpongeza Makamo wa pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa umahiri wake mkubwa wa kuyasimamia vyema majukumu ya Wizara zote za Serikali.

Vile vile nimshukuru sana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu), pamoja na watendaji wake wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii. Lakini pia kwa namna ya upekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi zao nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za kamati, jambo ambalo imekuwa ni wepesi kwangu kuweza kuiongoza kamati hii. Wajumbe wameonesha umahiri na umakini wa hali ya juu, na wameweza kuijadili ipasavyo bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa maslahi mapana kwa ajili ya wananchi wetu wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu,

nasi hatuna budi kurejesha imani kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipeee naomba niwatambua Wajumbe wa kamati ya Kusismamaia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Omar Seif Abeid | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Panya Ali Abdallah | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Ame Haji Ali | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Mussa Ali Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Mtumwa Suleiman Makame | Mjumbe |

Aidha kamati hii inafanyakazi na makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yametupatia mafanikio makubwa. Makatibu hao ni:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Kassim Tafana Kassim | Katibu |
| 2. | Ndg. Karima Abdul-Wahab | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Ni jukumu la msingi la Kamati yetu kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu makadirio ya Wizara katika mapato na matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika kanuni ya 96(1), kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mnamo tarehe **03/05/2017,** na leo hii, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha **2017/2018.**

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo, naomba nitekeleze jukumu nililopewa na Kamati la kuwasilisha maoni ya Kamati, mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ina mafungu mawili tu ambayo ni vote ya **A01**- Ofisi ya Rais Ikulu, na vote ya **A02**-Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, na imepanga kutekeleza Program kuu tano zenye Programu ndogo (11), ambazo kwa ujumla zitajumuisha shuhuli zote zinazokusudiwa kufanywa ndani ya mwaka huu wa fedha, kama inavyoonekana katika kitabu kikuu cha Bajeti.

PROGRAMU NDOGO YA KUSIMAMIA HUDUMA NA SHUGHULI ZA MHESHIMIWA RAIS.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya **Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais**, inasimamiwa na Ofisi ya faragha ambayo pia inajukumu la kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo yaliyotolewa na **Mheshimiwa Rais**, na usimamizi wa nyumba za mapumziko anazozitumia **Mheshimiwa Rais.** Kwa ujumla, kamati yangu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na ofisi ya faragha ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpainduzi, katika kufuatilia ahadi zinazotolewa na Kiongozi wetu Mkuu wa Nchi katika maeneo tofauti, ambapo kwa mwaka **2016/2017**, jumla ya ahadi **60** zilifuatiliwa na kutekelezwa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Faragha kama inavyoonekana katika kitabu kikuu cha bajeti.

**Aidha,** Kamati yangu imefurahishwa na ongezeko la bajeti kwa mwaka **2017/2018**, katika miradi wa maenedeleo ambayo nayo pia inasimamiwa na Ofisi ya faragha, yenye lengo la kuboresha majengo yanayotumiwa na **Mhesimiwa Rais**. Ni ukweli usiofichika kuwa, kukaratabati majengo ya Ikulu ambayo mengi yao ni ya muda Mrefu, kunahitaji fedha nyingi, ili kuhakikisha asili na haiba ya majengo hayo haipotei.

**Mheshimiwa Spika,**

Mbali na pongezi hizo kwa ofisi ya faragha ya **Mheshimiwa Rais**, kamati yangu inasisitiza juu ya mazingatio ya tatizo la mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu ya Mkoani, ambayo katika bajeti hii haijatengewa fedha yoyote, ikiwa ni hivi karibuni tu, kutokana na mvua

za masika zinazoendelea kunyesha, Ikulu ya Mkoani imeathirika kwa kuongezeka athari za mmong'onyoko zilizoanza kujitokeza hapo mwanzo, ambapo kamati yetu, pamoja na mambo mengine, wakati ilipotembelea katika eneo hilo, iliagiza na kusisitiza juu ya udhibiti wa eneo hilo ufanyike haraka kabla ya athari kubwa haijatokea.

Hata hivyo, kamati yangu inashauri kutengwe fedha katika bajeti hii, ili kutatua tatizo hilo kabla athari hizo hazijawa kubwa zaidi. Aidha kwa bajeti ya mwaka ujao wa fedha, kamati inasisitiza kuwa, tatizo hilo lipewe kipaumbele ili kuhakikisha kadhia hio inakwisha kabisa kwa Majengo yetu yaliyoonesha kupata athari.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya pili ni ya kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi, ambayo inakusudia kuendeleza taswira nzuri baina ya **Mheshimiwa Rais** na Wananchi wake. Kamati yangu imeridhika na makadirio yaliopangwa katika programu hii, hata hivyo Kamati inapendekeza baadhi ya mambo, kwa lengo la kuimarisha zaidi suala la kumtangaza **Rais** wetu, na kumfanya awe karibu zaidi na wananchi anaowatumikia. Suala la mwanzo ni kuongeza juhudi za makusudi katika kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na wananchi, kwa kuhahakisha kwamba, shughuli anazozifanya **Mheshimiwa Rais**, zinaandaliwa vipindi maalum, aidha kupitia **TV**, radio au mitandao ya kijamii. Suala hili ambalo linafanyika kwa sasa, lakini kamati inaona bado jitihada zaidi zinahitajika kuongezwa, kwa kuwa mahitaji ya vipindi hivi vya kumtangaza Rais, bado havijakidhi

haja ipaswavyo, kwani wananchi walio wengi katika maeneo ya vijijini, hawapati habari za mambo mazuri yanayofanywa na Rais wao.

Aidha kamati inaomba na kushauri idara hii, ikusudie kuwafikia idadi kubwa zaidi ya wananchi, sio tu ndani ya Zanzibar, bali hata nje ya nchi, ambapo mitandao ya kijamii inatumika kwa kiasi kikubwa. Jambo hili, litaleta muelekeo mzuri, si kwa ajili ya kumtangaza Rais pekee, bali pia litatoa muelekeo mzuri wa nchi yetu yote kwenye jamii za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inasisitiza pia, matukio mbali mbali ya kihistoria yanayohusu viongozi wetu wakuu na nchi kwa ujumla, yatangazwe na yatengenezewe vipindi maalum, ili wananchi wa rika mbali mbali, waweze kujuwa historia ya nchi yao vizuri. Kufanya hivi kutasaidia kuepusha taarifa za upotoshaji dhidi ya Viongozi wetu, sambamba na kuliwezesha rika la vijana kuifahamu vyema historia ya nchi yetu, wapi tulipotoka, wapi tulipo sasa, wapi tunaelekea na kuwataka vijana kuiunga mkono Serikali iliyopo madarakani na kuachana na maneno ya watu wachache ambao hawaitakii mema nchi yetu.

**PROGRAMU YA KURATIBU USHIRIKIANO WA KIKANDA, MASHIRIKA YA KIMATAIFA NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE NCHI.**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina lengo la kuiwezesha Zanzibar kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kikanda na kimataifa, na kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa lengo la kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuona azma ya kuwepo kwa idara ya uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje, inazaa matunda, kamati yangu inashauri kwamba, jitihada zaidi ziongezwe katika kuwavutia wawekezaji wenye asili ya Kizanzibar, kuja kuwekeza katika sekta mbali mbali ikiwa ni pamoja na sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika**,

ili kuona azma hii inafikiwa, kamati inashauri maazimio yatokanayo na kongamano la diaspora linalofanyika kila mwaka yanafanyiwa kazi, ili kujenga imani kwa Wazanzibar na Watanzaia kwa Ujumla wanaoishi nje ya nchi na hatimae kuongeza ari ya uekezaji na kuitangaza Zanzibar zaidi katika soko la Utalii katika maeneo mbali mbali ulimwenguni.

## PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA OFISI YA RAIS IKULU.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa malengo ya programu ndogo zilizo chini ya Programu kuu hii, ni pamoja na kuimarisha shughuli za mipango, kuandaa na kuchambua sera na utafiti pamoja na kuimarisha uwezo wa kiutendaji na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**,

Zanzibar ni sehemu ya Afrika Mashariki, lakini ni ukweli usiofichika kuwa, bado muamko wa wananchi wetu kutumia fursa zitokanazo na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni mdogo mno. Wananchi bado hawajawa na muamko wa kutumia fursa za kiuchumi na kijamii zinazopatikana kutokana na uwepo wa jumuiya hii, na hii sio kwa kuwa hawahitaji kutumia fursa hizo, lakini ni kwa sababu ya kukosa taarifa muhimu na za msingi zinazohusu jumuiya hiyo. Ushahidi wa haya pia unaweza kuonekana kupitia wahitimu mbali mbali kutoka vyuo vya Zanzibar, ambao wanaifahamu Jumuiya hiyo katika nadharia tu, lakini si katika uhalisia wake.

Aidha, kwa kua Idara ya Uendeshaji na Utumishi, inayosimia programu kuu hii ya **Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu, inajihusisha pia na kufanya tafiti mbali mbali,** kamati yangu inashauri utafiti ambao unakusudiwa kufanywa na ORMBLM kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kuhusu fursa zinazopatikana katika soko la Afrika Mashariki, chini ya programu ndogo ya Uratibu wa Shuguli za Mipango, Sera na Utafiti,

ukusudie pia kuhamasisha jamii ya Kizanzibar, hususan vijana kuchangamkia fursa za jumuiya Afrika Mashariki, ambazo kwa ujumla Zanzibar inaonekana kufaidika nazo kwa kiasi kidogo sana.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo nyengine ni ya **Kuratibu na kusimamia shughuli za usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi-Pemba** ambayo ina lengo la kuimarisha uwezo wa kiutendaji  na uratibu wa shughuli za ORMBLM. Kabla sijatoa maoni ya kamati kwa eneo hili, kwa niamba ya Kamati yangu, naomba kwanza nichukue fursa hii, kumpongeza Afisa Mdhamini katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Bi. Jokha Khamis Makame,** kwa kazi nzuri iliyofanyika chini ya usimamizi wake, katika kuyafanyia marekebisho makubwa majengo yaliyo ndani ya ikulu ya Chake na Micheweni, na hatimae kurejeshaha haiba yote ya eneo hilo.

**Mheshimiwa  Spika**,

Kilichofanyika kupitia Ofisi ya Ofisa Mdhamini-Pemba, ni mafanikio ya kupigia mfano na kuigwa na Viongozi pamoja na watendaji wengine wa Serikali wanaokabidhiwa majukumu ya usimamizi wa nyadhifa mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Nidhamu ya hali ya juu katika matumizi ya fedha, ndio kitu ambacho kamati yangu inakiona ikitazama ukarabati huo mkubwa uliofanyika. Aidha, kwa kuwa bajeti ya

shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeongezeka, kamati inasahuri kutoicheleweshea fedha, Ofisi ya Afisa mdhamini-Pemba, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo nyengine ambayo kamati yangu imeitolea maoni ni Programu ya **Usimamizi wa Usalama wa Uatumishi wa Umma, (GSO)**ambayo lengo lake ni kuimarisha shughuli za upekuzi kwa watumishi wa umma, kabla na baada ya kuajiriwa. Kwa ujumla, utendaji wa kazi wa idara hii naweza kusema kwamba ni wenye mafanikio pamoja changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika utendaji kazi wa idara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Idara ya GSO ni miongoni mwa Idara zenye mazingira magumu ya utendaji kazi, kunakotokana na madhaifu ya kisheria, lakini pia kuwepo na changamoto ya ufinyu mkubwa wa Bajeti. Kamati yangu, katika kutazama kwa ukaribu viashiria vya matokeoa kwa idara hii, imebaini kuwa, Idara haikufikia malengo yake, katika shuhuli nzima ya kufanyia upekuzi wafanya kazi wa Serekali, ambapo imefanikiwa kuwafanyia upekezi wafanya kazi 30 tu kati kati ya 100 waliokadiriwa katika mwaka 2016/2017. Aidha, malengo sawa na hayo yamepangwa kwa mwaka 2017/2018, ambapo kamati yangu ina hofu ya kutofikiwa matarajio hayo kama ilivyokuwa kwa mwaka 2016/2017, kwa kuwa bado idara hii ina changamoto za kisheria ambazo bado hazijafanyiwa kazi. Maoni ya

Kamati yangu ni kwamba jitihada za makusudi zichukuliwe, ili mapungufu ya kisheria ambayo mwaka uliopita yalisababisha kutofikiwa kwa lengo, yaweze kuondolewa

**Mheshimiwa Spika.**

Serikali ya Mapimduzi ya Zanzibar imekua na sera na Sheria nyingi ambazo zinatekelezwa na Wizara au taasisi mbali mbali. Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Miongoni mwa idara muhimu ambazo jukumu lake la msingi ni kufanya tathmini ya Sera na Sheria mbali mbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kamati yangu imebaini kuwa, baadhi ya changamoto za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, zinatokana na mapungufu ya kisheria, ambayo pia hupelekea changamoto ya kukosekana bajeti ya kutosha kwa baadhi ya idara zake. Hii ni pamoja Sheria inayosimamia kuwepo kwa **GSO-Zanzibar**. Hivyo kamati yangu kupitia programu kuu ya ya Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu, kati ya sheria na sera mbili ambazo zimepangwa kupitiwa ndani ya mwaka wa fedha 2017/2018, Sheria inayosimamia **GSO** ipewe kipaumbele ili kuondoa changamoto zinazoikabili Idara hiyo, ikiwa ni pamoja changamoto ya Ufinyu wa bajeti ya uendeshaji wa ofisi hiyo kwa hapa Zanzibar, kwani idara ya GSO ni Idara muhimu kwa mustakabali wa Serikali zetu kwa ujumla

## OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

**Mheshimiwa Spika.**

Kamati yangu kwa umakini pia, imepitia Fungu A02-Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ambalo lina Programu ya usimamizi wa Majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu, na Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAJUKUMU YA KIKATIBA NA KISHERIA YA BARAZA LA MAPINDUZI NA KAMATI YA MAKATIBU WAKU.**

**Mheshimiwa Spika,**

Chini ya programu hii kuu, Kamati yangu, imepatiwa ufafanuzi juu ya kitengo cha Tehama ambacho kwa mwaka 2017/2018, hakionekani kutengewa fedha kutoka ofisi ya Baraza la Mapinduzi, kunakotokana na kukamilika kwa shughuli nyingi zilizopangwa kufanywa na kitengo hicho ndani ya mwaka **2016/2017**, ikiwa ni pamoja na uwekaji wa huduma za Internet na camera za ulinzi.

Aidha kamati yangu inashauri, katika kuimarisha usalama zaidi wa Ofisi za Baraza la Mapinduzi, suala la uimarishaji wa camera za CCTV za ulinzi lizingatiwe, kwa kuwa camera hizo zipo tayari kwa sasa. Hivyo Ofisi itafute namna ya kupata fungu maalum kwa ajili ya kuzifanyia "*maintenance*" camera hizo, kwa lengo la kuziimarisha na kuzifanya ziendelee kutumika kwa muda mrefu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika programu kuu hii pia, kuna pogramu ndogo ya **Tathmini ya Utendaji Kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma**, ambayo inakususdia kuhakikisha malengo ya kila wizara na taasisi za Serikali, yanatekelezwa ipasavyo na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**,

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya taasisi za Serikali, kupitia watendaji wasiofuata miongozo ya utumshi wa umma, kulalamikiwa juu ya kutowahudumia vizuri wananchi wanaofika katika taasisi hizo, ili kupatiwa huduma. Aidha katika utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2016/2017 kumeelezwa kuwa jumla, ya Wizara **13** zimefuatiliwa katika utekelezaji wake wa Sera, sheria, miongozo na maagizo ya Serikali. Hivyo kamati yangu inashauri ufuatiliaji huo wa taasisi za Serikali, uzingatie pia nidhamu na uwajibikaji wa baadhi ya watendaji ambao wanaonekana kuwa ni kikwazo kinachoweza kurudisha nyuma maendeleo na juhudi za Serikali.

**USHAURI WA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa ujumla, kamati yangu imeridhishwa na kuridhia bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo ni jumla ya Tsh. **6,634,700,000** kwa

fungu la **A01**, na **Tsh. 1,707,900,000** kwa fungu la **A02**, ziliyoambatana na ufafanuzi wa mipango mbali mbali ya mwaka mzima. Aidha, kamati yangu inasisitiza kuwa, nidhamu ya hali ya juu na ari ya uwajibikaji inahitajika katika matumizi ya fedha za umma zilizoainishwa na Wizara hii katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

**Hitimisho:**

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maoni hayo ambayo yamejikita katika programu kuu na ndogo zilizo na umuhimu zaidi kwa kamati yangu, ili kuhakikisha wizara hii inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, ni imani ya kamati yangu kuwa, baada ya hutoba nzuri iliyosomwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na maoni haya ya kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nawaomba wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu, waichangie vyema bajeti hii, kwa lengo la kupata utekelezaji bora wenye maslahi kwa wananchi wetu.

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena, wewe binafsi, **Mheshimwa Spika**, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti

hii, ili wamuwezeshe Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wakuu wa Kitaifa, naiunga mkono hoja kwa asliami 100%.

**Naomba kuwasilisha**

……………………

Mhe. Panya Ali Abdalla

Kny: Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**